



## BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI (CRB) TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO 2015 HADI 2020



Muonekano wa maendeleo ya ujenzi wa jengo la CRB kabla ya kukamilika katika eneo la NCC Link Dodoma.



Muonekano wa jengo la CRB litakavyokuwa baada ya kukamilika katika eneo la NCC Link Dodoma.

kutoka 4,021 mwaka 2015 hadi 5,414 mwaka 2020.

Bodi imeongeza idadi ya kazi zinazotolewa kwa mwaka na idadi ya washiriki imeongezeka kunatokana na Serikali ya Awamu ya Tano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020. Hii inaonyesha kuwa ujenzi wa ndani ili waendeleo kunufaika na zabuni za miradi mikubwa.

### 3.2. Ubia

Bodi imeendelea kuhimiza Ubia ili kuwezesha Makandarasi wa ndani kushiriki katika utekezaji wa miradi mikubwa inayotokana na uwekezaji wa Serikali ya Awamu ya Tano ili faida kubwa inayotokana na uwekezaji huo ibaki hapa nchini na kusaidia uchumi wa nchi yetu tofauti na kama miradi hiyo yote ingefanywa na Makandarasi kutoka nje kwani manufaa yote yangeenda kwenye uchumi wa nchi zao.

### 3.3. Ushiriki wa Makandarasi katika Miradi mikubwa ya Serikali.

Katika kipindi cha Serikali ya awamu ya tano, Bodi imeshuhudia uwekezaji mkubwa wa Serikali katika ujenzi wa miundombinu mbali mbali. Ni kipindi ambacho imefanyika miradi mingi mikubwa ambayo thamani yake kifedha haijawahi kushuhudiwa katika nchi yetu.

Miradi hii mikubwa inatekelezwa na Makandarasi wa kigeni na pia wa ndani. Utekezaji wa miradi hii mikubwa ni fursa kubwa ya kazi kwa Makandarasi. Pale miradi inapotekelezwa na Makandarasi wageni, Makandarasi wa ndani hushiriki kwa kufanya kazi kama "subcontractors"

katika miradi hiyo.

Ushiriki wa Makandarasi wa ndani katika miradi mikubwa ni muhimu sana kwa kuwa ukiacha faida za kipato kwa Makandarasi husika, Makandarasi wa ndani hujifunza teknolojia mpya na ujuzi na mbinu mpya za utekezaji wa miradi mikubwa. Hii inamaanisha kwamba kwa siku za usoni, miradi mikubwa itakuwa inatekelezwa zaidi na Makandarasi wa ndani na hivyo fedha nyingi za miradi hiyo kubaki nchini kwetu kwa faida ya uchumi wa nchi yetu.

**Baadhi ya miradi mikubwa iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo;**

- Reli ya kisasa kutoka Morogoro hadi Makutupora, Dodoma
- Reli ya kisasa kutoka Dar

es salaam hadi Morogoro

- Mradi wa kufua umeme Kinyerezi
- Daraja la kigongo – Busisi
- Maboresho ya Bandari ya Dar es salaam
- Usambazaji wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Igunga
- Daraja jipya la Salender
- Ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka kutoka Kariakoo hadi Mbagala
- Barabara za juu "Ubungo Interchange"
- Ujenzi wa mradi wa umeme katika maporomoko ya Rusumo.

**Katika kipindi hiki, iko miradi miwili ya barabara iliyotengwa mahsusi kwa lengo la kukuza uwezo wa makandarasi wa ndani. Miradi hiyo ni;**

- i. Ujenzi kwa Kiwango cha lami wa barabara ya Kaliua – Urambo (km 28) inayojengwa kwa ubia na

Makandarasi M/s Salum Motor Transport Co. Ltd, M/s Annam Road Works Co Ltd na M/s Jossam Company Ltd.

ii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Rudewa – Kilosa (km 24) unaotekelezwa na kampuni ya Umoja Kilosa JV ambayo ni ubia wa Makandarasi M/s Kings Builders Ltd, M/s Comfix & Engineering Ltd, Emirate Builders Co. Ltd, Halem Construction Company Ltd, Audacia Investment Ltd na Pioneer Builders Ltd.

**Aidha wapo Makandarasi wa ndani wanaoendelea na ujenzi wa miradi mikubwa kama vile;**

- i. M/s Nyanza Road Works (ujenzi wa barabara ya Bulamba – Kisorya, Km 51)
- ii. M/s Nyanza Road Works (ujenzi wa barabara ya Nyakanazi – Kibondo Km,50)
- iii. M/s Estim Company

Ltd (Upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha, Km 19.1 kutoka njia mbili hadi nane pamoja na upanuzi wa madaraja ya kibamba, Kiluvya na Mpiji)

iv. M/s Mayanga Contractors Compnay Ltd. (Ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Chato).

### 3.4. Mfuko wa kusaidia Makandarasi (CAF – Contractors Assistance Fund).

Katika jitihada za kuendeleza Makandarasi, Bodi imeendelea kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi wa ndani ili kuwawezesha kupata dhamana katika mabanki bila ya rehani kitu chochote.

Mpango huu unatoa dhamana kwa ajili ya zabuni (Bid Security) na malipo ya awali (Advance Payment Guarantees) kwa Makandarasi wadogo na wa kati (Madaraja ya 4 – 7 kawaida na 2-3 maalum).

Aidha katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 Makandarasi 1,168 wamenufaika na huduma za mfuko huo.

Bodi inaona mfuko huu ni muhimu hususan katika kipindi hiki kwani unawawezesha Makandarasi wanaopata miradi inayotokana na uwekezaji wa serikali katika miundombinu mbali mbali kupata dhamana na kuwawezesha kushiriki katika zabuni mbali mbali na pia kupata fedha za kuanzia utekezaji wa miradi kwa urahisi zaidi.

### 4. Kukua kwa Uwiano wa Makandarasi wa ndani katika Soko la kazi za ujenzi.

Kupitia usajili wa miradi ambao hufanywa na Bodi kwa lengo la kukusanya takwimu, uwiano wa soko la kazi za ujenzi kwa Makandarasi wa ndani umeongezeka kutoka 40% mwaka 2015 hadi 52% mwaka 2020.

Hii ni ishara kwamba Makandarasi wa ndani wanashiriki vyema katika miradi mbali mbali inayotokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali ya awamu ya Tano katika miundombinu. Makandarasi wa ndani wameshiriki miradi hiyo moja kwa moja au kupitia kwa Makandarasi wa kigeni kwa kufanya kazi kama "sub contractors".

### 5. Ujenzi wa Ofisi za Bodi Dodoma.

Katika kutekeleza azma ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhamishia makao Makuu ya Serikali jijini Dodoma, Bodi imeweza kujenga jengo la ofisi zake za makao Makuu lenye sakafu 11 katika eneo la NCC.

Ujenzi wa jengo hili ni mafanikio kwa Bodi na yametokana na maamuzi sahihi ya Serikali ya awamu ya Tano kuhamishia Makao Makuu jijini Dodoma ambapo ilizihimiza taasisi zenye uwezo wa kujenga majengo yake kufanya hivyo.

Kwa maamuzi hayo sahihi, Bodi imepata jengo lake ambalo litatumika kwa matumizi yake pamoja na kuzipangisha taasisi



Muonekano wa maendeleo ya ujenzi wa barabara za juu Ubungo jijini Dar es Salaam. (Ubungo Interchange).